SHULE YA SEKONDARI CHIEF KIDULILE,
S .L. P. 95,
LUDEWA.
29/03/2022.

Namba za simu Kwa mawasiliano zaidi:
Mkuu wa Shule: **0753-014-449**
Makamu Mkuu wa Shule :- **0752-367553**
Patron **:- 0769143848, Matron 0753464387,0764889404**
MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI: ……..
S. L. P. …….
…….

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI CHIEF KIDULILE WILAYA YA LUDEWA MKOA WA NJOMBE MWAKA 2022.

1. Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha TANO katika shule ya sekondari CHIEF KIDULILE mwaka huu 2022. Shule hii ina tahasusi ya CBG, HGL na HGE ni ya Wavulana na Wasichana, ni ya bweni . Shule ipo nyanda za juu kusini mwa Tanzania. Shule hii ipo Wilaya ya Ludewa km 1 toka makao Makuu ya Wilaya,ipo umbali wa km 160 kutoka mjini Njombe (Makao Makuu ya Mkoa Njombe) usafiri wa kutoka Mji wa Njombe unapatikana katika kituo cha mabasi Njombe Mjini. Nauli ni Tsh 12,000/=. Unaweza kutumia basi la Hausung,Ibu,au Kijosho ambayo yote yanafika Wilayani Ludewa,Shuleni pia kuna huduma zote za maji,simu na umeme. Hospitali ya Wilaya ipo km 2 toka shuleni.

Muhula wa masomo unaanza tarehe …… Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe …… mwisho wa kuripoti ni tarehe …….

KAULI MBIU YA SHULE HII: ELIMU NI MTAJI WA KUDUMU (EDUCATION IS AN EVERLASTING CAPITAL)

2. MAHITAJI MUHIMU

Yafuatayo ni maagizo / mahitaji , michango na vifaa muhimu ambavyo ni lazima uje navyo siku utakapo fika shuleni.

A: FEDHA

i. Mchango wa karo ya shule Tshs 70,000/= kwa mwaka.
ii. Ukarabati wa samani Tsh 20,000/=
iii. Taaluma Tshs 20,000/= kwa mwaka.
iv. Kitambulisho na picha Tsh 6,000/=
v. Matibabu Tshs 20,000/= kwa mwaka
vi. Tahadhari Tshs 5,000/= (haitarejeshwa)
vii. Mahafali Tsh 10,000/=
viii. Mchango kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na wafanyakazi wengine Tsh 30,000/=
ix. Ukarabati wa majengo Tshs 5,000/=
x. Nembo ya Shule Tsh 2,000/=

JUMLA TSHS 188,000/= ikiwemo Karo na michango mingine.

Fedha zote (i – ix) ziwekwe NMB A/C namba 60101200043 kwa jina la CHIEF KIDULILE SECONDARY SCHOOL, Shuleni iwasilishe nakala halisi ya "bank pay in slip" siku ya kuripoti shuleni

B. SARE YA SHULE (NGUO RASMI ZA SHULE)

A: WAVULANA

i. Suruali mbili za damu yam zee zenye mshono wa heshima (zisiwe kata k),zisiwe pana sana, finyu sana chini wala zisiwe fupi.
ii. Mashati mawili meupe (Tetroni) mikono mirefu yanayo weza kuchomekea ndani.
iii. Jozi mbili za soksi nyeupe
iv. Sweta rangi ya damu yam zee inapatikana shuleni kwa Tsh 12,000/=
v. T-shirt ya shule inapatikana shuleni kwa Tsh 15,000/= yenye Nembo ya Shule

NB: Kitambaa cha suruali kimeambatanishwa.

B: WASICHANA

i. Vigauni viwili (2) vyeupe vya soro ambayo haina marinda shingo duara, suruali mbili (2) za damu ya mzee.
ii. Jozi mbili ya soksi nyeupe.
iii. Viatu vyeusi vya ngozi na visiwe na kisigino kirefu na view vya kufunga kamba na vya kupiga kiwi, jozi mbili (2) visiwe vya plastiki (yebo).
iv. Sweta rangi ya damu yam zee na T-shirt inapatikana shuleni kwa Tsh 15,000/=

NB: Kitambaa cha suruali kimeambatanishwa.

C: MAVAZI NJE YA DARASA

Kila Mwanafunzi aje na jozi mbili za track suti rangi nyeusi zenye mistari myeupe pembeni, suruali ya dark blue kwa wavulana na sketi dark blue kwa Wasichana kama shamba dress.

NB: Kitambaa cha shamba dress kimeambatanishwa.

D: VIFAA

1. Unatakiwa kuja na godoro la Inchi 2½ .
2. Mashuka mawili rangi ya pink, blanketi moja , mto na foronya lake la pinki na taulo.
3. Uje na vyombo vya chakula : sahani moja , kikombe , kijiko cha chakula .
4. Ndoo ya lita 20 ambayo itatumika kwa matumizi binafsi ya Mwanafunzi.
5. Bunda la karatasi mbili za karatasi (ream) A4 standard (WHITE) yaani bunda 1 kila muhula.
6. Daftari za kutosha , mkebe wenye vifaa (mathematical set) na pia scientific calculator uwezo kuanzia f (x) 82 kwa HGL na CBG/HE f(x) 991.
7. Faili moja kwa ajili ya maendeleo yako , litakabidhiwa wakati wa kusajili.
8. Nguo za michezo , T – shirt bluu yenye mistari myeupe pembeni , bukta nyeusi, viatu / raba na soksi za michezo.
9. Uje na kwanja (fyeko) na jembe lenye mpini na **SABUNI YA MAJI NZITO LITA TANO (5), NA SIO FEDHA KWANI FEDHA HAITAPOKELEWA** pamoja na mfagio hard bloom.
10. Sanduku imara kwa kuhifadhia vifaa vya Mwanafunzi ni muhimu
11. Sanduku imara kwa kuhifadhia vifaa vya Mwanafunzi ni muhimu Hutapokelewa bila kuonyesha " Leaving Certificate na result slip"
12. Uje na chandarua (Mosquito net).

MUHIMU: Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo nyingine aina yeyote kwani hakuna muda wa kuzivaa hapa shuleni . Pindi mwanafunzi anakuja kuripoti aje amevaa track suti nyeusi na isiwe

imembana kwa wasichana na kama anamatatizo ya kifua basi tunashauri anunue track suti nyeusi ambayo ni nzito.

NB: Vifaa vyote vitakaguliwa kabla hujaingia bwenini

E: MAELEKEZO MUHIMU

(i) Ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na simu shuleni au kutumia simu akiwa shuleni . Simu itakayo kamatwa haitarudishwa kwa Mwanafunzi badala yake itavunjwa mbele ya hadhara na Mwanafunzi mhusika kusimamishwa au kufukuzwa shule.

(ii) Usifike bwenini bila ya kuripoti Ofisini.

(iii) Mwanafunzi asije na kifaa chochote kinacho tumia umeme kama radio, simu, mashine za kunyolea n.k.

(iv) Mwanafunzi hatapokelewa endapo hatakamilisha michango na vilevile ahadi ya kulipa baadae haitasikilizwa.

(v) Kuwa na nyele fupi mda wote (kusuka hairuhusiwi).

(vi) Ni marufuku kuja na pete, herein, kofia, mzula, rangi za kucha na mdomo na saa zenye urembo.

(vii) Fomu zilizoambatanishwa zijazwe sehemu husika na zitakabidhiwa wakati wa usajili.

(viii) Heshimu watu waote.

(ix) Zingatia matumizi bora ya mali na muda.

(x) Vifaa vya muziki pia haviruhusiwi

(xi) Mwanafunzi ataruhusiwa kutoka nje ya shule jumapili ya mwisho wa mwezi

(xii) Mwanafunzi haruhusiwi kuja na vyakula shuleni.

F. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule itaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya elimu Nchini.

Unatakiwa kuxingatia mambo ya muhimu yafuatayo ambayo yatafafanuliwa lwa maandishi na utapewa nakala mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila kazi za ndani na nje ya darasa.

(c) Kuwahi katika shughuli nyingine utakazo pewa.

(d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi katika shule.

(e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.

(f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

(g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

(h) Huruhusiwi kuwa na simu wala kamera.

NB: KILA MWANAFUNZI ACHUKUE TAHADHARI DHIDI YA UGONJWA UNAOTOKANA NA VIRUSI VYA CORONA .

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE.

1. Wizi
2. Uasherati , ubakaji na ushoga
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
4. Uvutaji bangi.
5. Makosa ya jinai.
6. Kupigana au kupiga.
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
8. Kudharau bendera ya Taifa.
9. Kuoa au kuolewa.
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
11. Kutoa mimba.
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi.

IMEANDALIWA NA :

.....

BARA KIHAGA

MKUU WA SHULE

PHONE 0753 - 014449

ORODHA YA VITABU VYA MASOMO.

CHEMISTRY:

1. Advanced chemistry review by William .W. (Mzumbe book shop project, 2014)
2. Physical chemistry by Delungu, (Mzumbe book shop project, 1998).
3. Advanced level inorganic chemistry part I and II (Tanzania instate of education, 1995)
4. Organic chemistry volume I . The fundamental principles I. L(Longman ltd 1990)

GEOGRAPHY:

1. Principle of physical geography by F.J Monk house.
2. Geography. Integrated approach by D Waugh.
3. Practical geography for Africa by J.M Pritchard.
4. General geography in diagram by R.B Bunnert.
5. Simplified physical geography (A – Level) by D.M.
6. Statically methods and the geographer by S. Gregory.
7. Certificate physical and human geography by Goh Chang Leong

BIOLOGY:

1. New understanding biology by Suzan Toole.
2. Advanced biology principle and application by C.J Clegg and D.G Mackean.
3. Advanced biology by Michael Kent.
4. Biology S. Chand 2008 class XII, Dr p.s Verma and Dr B.P panday.
5. Biology S. Chand for class XI.
6. Biology guide to dissection HGQROWETT.

GENERAL STUDYIES :

1. General Studies for A – Level Certificate for form five.
2. Contemporary approach A- Level general studies Notes for form five and six
3. General studies supplementary book for A-Level and colleges.

HISTORY:

HISTORY I AND II

1. Advanced leaners, history form 5 and 6 (history I and II) Mwandishi : Oxford year:2011 (current syllabus).
2. Advanced level : history for Africa, from Neolithic Revolution to present , Mwandishi : Zisti Kamali year: 2010.
3. Mastering advanced level : history year : 2011
4. Major events in the world history year : 2011
5. Advanced history paper 1 & 2
6. Advanced level for 5 &6 , Mwandishi : Nyambari Nyangwine year 2007.

ENGLISH :

1. Advanced level, literature from 5&6
    (i) Styslitics & communications . Theory of literature, novel , play and poetry, Mwandishi : Nyambari Nyangwine Godfrey Rutta Bukagile
    (ii) Literature test book for advanced levels. Analyses of literature works, Mwandishi : M.Kadege year 2005.

PLAYS:

(i) Betrayal in the city , Mwandishi: France Imbuga
(ii) I Will Marry when we want, Mwandishi : Ngugi wa Thiongo & Ngugi wa Mirii.
(iii)The bride, Mwandishi : Austin Bukeya.
(iv)Lwanda Magere, Mwandishi: Okoti Omatatah
(v) An Enemy of the people, Mwandishi: Henrik Ibsen
(vi)Black Mamba, Mwandishi : John Ruganda.

NOVEL AND SHORT STORS.

(i) Encounters from Africa , Mwandishi: Macmillan Education Limited.
(ii) The beautiful ones are not yet born, Mwandishi : Ayi Kwei Armah
(iii)A man of the people, Mwandishi: Chinua Achebe
(iv)Divine providence, Mwandishi: Severin N. Ndunguru.
(v) The rape of the peal , Mwandishi: Magal Nyago
(vi)Vanishing Shadows, Mwandishi : Namige Kayonda 7
(vii) His Excellency the head of state, Mwandishi : Damy Safo.
(viii)Season of waiting , Mwandishi : Davido Omowale.

POETRY:

1. Selected poems, Mwandishi : Tanzania Institute of Education (TIE).
2. The wonderful surgeon and other poems, Mwandishi : Charles Mloka.

ECONOMICS 1

1. Introduction to economics ; stanlake,g.f and grant s. f 6_{th} edition (esse longman group limited 1995).
2. Modern microeconomics : analysis and applications : hyman david , 2_{nd} edition (Homewood : Irwin 1989)
3. Success in Economics : Lobley derrick (1983).

ECONOMICS II

1. Economic for a developing world : 3_{rd} edition. Todaro M.P (London longman 1992).
2. International money theory, finance and instition hallwood p and macdonald r (New York Basil black).
3. Our problems our solution an economic and public policy agenda for Kenya: Gathern w and shaw r (eds) (Nairobi Institute of Economics affairs 1998)
4. Ambilikile I & II.

Tafadhari jaza fomu zifuatazo kabla ya kufika shuleni.

(a) Medical Examination form ambazo itajazwa na Mganga mkuu wa hospitali ya serikali.
(b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi /Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
(c) Fomu ya wazazi kukiri kukubaliana na sheria na kanuni, kulipa ada michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

NB: *i) Fomu hizi zitakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara baada ya kuripoti shuleni .*
ii) Mwanafunzi aandaliwe Cheti cha kuzaliwa mara atakapojiunga na Sekondari (kama bado)

Imeandaliwa na,

BARA KIHAGA
MKUU WA SHULE
0753 – 014449

SHULE YA SEKONDARI CHIEF KIDULILE
TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI KIDATO CHA V – 2022.

1. Jina Kamili ……
2. Mahala alipozaliwa …….
3. Tarehe ya kuzaliwa ……
4. Jina la baba ……..... hai / marehemu …….
   Kazi …… Namba za simu …….
5. Jina la mama …… hai / marehemu …….
   Kazi …… Namba za simu ……
6. Je baba na mama wanaishi pamoja ? …… kama ni hapana
   Wewe unaishi na nani ? ……
7. Jina la mlezi ……..... kazi ……
   Namba ya simu …….
8. Uhusiano na mlezi ……
9. Anwani ya mzazi / mlezi ……
10. Shule ya sekondari uliyotoka …….
11. Dhehebu /dini ……..
12. Wakati wa likizo utakuwa na nani na wapi ? Taja sehemu moja tu utakayo kwenda kila wakati
    ……. Anwani na namba ya simu …….
13. Je hapa Ludewa una ndugu ? mtaje na simu yake ……
    …….
14. Nathibitisha kuwa habari nilizotoa hapa ni kweli na sahihi .
    Sahihi ya Mwanafunzi …… Tarehe ……
    Sahihi ya Mzazi/Mlezi …….. Tarehe ……

SHULE YA SEKONDARI CHIEF KIDULILE

FOMU YA MAPATANO / KUKUBALI NAFASI YA MASOMO KIDATO CHA TANO MWAKA 2022.

AHADI YA MWANAFUNZI

Mwanafunzi ……

Anwani ……

Mimi ……

Nimekubali /sikubali kujiunga na jumuiya ya sekondari Chief Kidulile. Nimesoma maagizo ya shule kwa makini na kuyaelewa . Naahidi kuwa mtiifu na nitazingatia sheria / kanuni na kukubali adhabu iwapo nitakiuka sheria za shule hii ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

Sahihi ya mwanafunzi …….. ***Tarehe*** ……

AHADI YA MZAZI /MLEZI

Mimi …… Mzazi /Mlezi wa Mwanafunzi

…… Nimesoma kwa makini maagizo ya shule yaliyotolewa kwa motto wangu . Nimekubali / sikubali achukue nafasi hiyo. Naahidi kuwa nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumukuza na kumlea Mwanafunzi Kielimu na Kitabia . Naahidi pia kumlipia karo ya shule na michango mingine mbalimbali iliyoagizwa na shule kwa wakati mwafaka . Kinyume chake nichukuliwe hatua za kisheria.

Sahihi ya Mzazi / Mlezi ……. ***Tarehe*** ……

CHIEF KIDULILE SECONDARY SCHOOL,
P. O. BOX 95,
LUDEWA.
29/03/2022.

TO THE MEDICAL OFFICER,

……..

MR/MRS ……. (Full name)

Please examine the above student as to her/his physical and mental fitness for a full time student in this school.

The examination should have to involve the following categories .

1. Vision with glasses , right ……. Left.
2. Blood pressure …… haemoglobin ……
3. F.V. Bleeding ……
4. Urine for sugar, Albumin and pregnancy ……
5. Stool for routine examination ……
6. Venereal diseases ……
7. Neurosis ……
8. Any abnormality
   (a) Heart …….
   (b) Lung …….
   (c) Speech ……..
9. Are there any serious e.g leprosy, epilepsy, Asthma, Diabetes

   ……..

DOCTOR'S NAME & SIGNATURE

…….

Thank you,

…….

BARA KIHAGA

THE HEADMASTER